Mizigo Ya Maisha

na

Ellis P. Forsman

Mizigo Ya Maisha

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 7, 2011

Mizigo Ya Maisha

Wagal. 6:2,5

Wagal. 6:5, "*Maana kila mtu atalichukua furushi lake mwenyewe.*"

Wagal.6:2, "*Mchukuliane mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo.*"

Zaburi 55:22, "*Umtwike BWANA mzigo wako naye atakutegemeza, Hatamwacha mwenye haki aondoshwe milele.*"

Ni wajibu wa kila mwana damu popote pale kuwa na mizigo.

2 Wakor. 5:4, "*Kwa maana sisi tulio katika maskani hii twaugua, tukilemewa; si kwamba twataka kuvuliwa, bali kuvikwa, ili kitu kile kipatikanacho na mauti kimezwe na uzima.*"

Mizigo ya kindani na mizito maranyingi haionekani.

Watu wanapojaribu kubeba mizigo yao wenyewe inaweza ikawa vita vya kutisha nay a kipekee. Wanakuwa na mashaka kuhusu vitu; na mara nyingi mashaka yao yanaweza kusababisha athari zaidi kuliko vitu ambavyo wamekuwa wakiviwazia.

Imethibitishwa kwamba mashaka huvunja kinga ya ugonjwa, husababisha matatizo katika mfumo mzima wa chakula na moyo, vile vile na akili na mifumo mingine ya mwili. Ongeza katika hilo kutokuwa na furaha kutokana na kukosa usingizi kila kunapokucha na siku zilizoaribika.

Miaka kadhaa iliyopita, mtu aitwaye Repley aliorodhesha Gal. 6:2 na Gal. 6:5 kama maandiko yanayopingana.

Katika Gal. 6:2 neno "*mzigo*" linatokana na neno la Kiyunani "*baros*", linalo maanisha "mzigo." Hii inaweza kuwa "mzigo" au "kifurushi" cha ugumu, huzuni, au uchungu.

Lazima tuchukuliane mizigo yetu wenyewe ya namna hii.

Katika Gal. 6:5, neno "*furushi*" linatokana na neno la Kiyunani "*phortion*", inayo maanisha "chukua" ni ujumuisho wa wajibu wa mtu yeyote mbele za Mungu, ambayo kila mtu binafsi anahusika.

Ivyo, hii "chukua" inapaswa itofautishwe kutoka katika "mizigo" mizito ya msitari wa 2.

Biblia inatufundisha kufanya mambo matatu na mizigo yetu:

- Kubeba furushi letu wenyewe. Gal. 6:5, *Maana kila mtu atalichukua furushi lake mwenyewe.*"
- Kuchukuliana mizigo. Gal. 6:2, "*Mchukuliane mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo.*"

- Kumtwika Bwana mizigo yetu. Zaburi 55:22, "*Umtwike BWANA mzigo wako naye atakutegemeza, hatamwacha mwenye haki aondoshwe milele.*"

Kila Mtu Atauchukua Mzigo Wake Mwenyewe

Baadhi ya mizigo yetu haihamishiki.

Bwana amempa kila mwanadamu kazi yake mwenyewe.

- Marko 13:34, "*Mfano wake ni kama mtu mwenye kusafiri ameiacha nyumba yake, amewapa watumwa wake amri, na kila mtu kazi yake, naye amemwamuru bawabu akeshe.*"
- Gal. 6:4, "*Lakini kila mtu na aipime kazi yake mwenyewe, ndipo atakapo kuwa na sababu ya kujisifu ndani ya nafsi yake tu, wala si kwa mwenzake.*"

Hakuna mtu anayeweza kumwamini Bwana badala yako, au kuzitubia dhambi zako, au kukiri imani yako katika Yesu Kristo, au abatizwe badala yako. Hakuna awezaye kukufanyia majukumu yako ya Kikristo badala yako. Hakuna atakaye jibu mbele ya kiti cha enzi badala yako.

- Rum. 14:12, "*Basi ni hivyo, kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu.*"
- 2 Kor. 5:10, "*Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya.*"

Akuna mtu anayeweza kupotea ndani ya umati wa watu na kujificha nyuma ya wengine.

- Zabur. 33:13, "*Toka mbinguni BWANA huchungulia, huwatazama wanadamu wote pia.*"
- Ebr. 4:13, "*Wala hakuna kiumbe kisichokuwa wazi mbele zake, lakini vitu vyote vi utupu na kufunuliwa machoni pake yeye aliye na mambo yetu.*"

Kuchukuliana mizigo

Baadhi ya mizigo lazima tushirikiane na wengine.

Wafil. 2:4, "*Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo yaw engine.*"

Kila mara ni vizuri kuzingatia maneno katika maandiko jinsi yalivyo kaa. Ufunguo wa Gal. 6:2 inapatikana katika msitari wa 1.

Gal. 6:1, "*Ndugu zangu mtu akighafilika katika kosa lo lote, ninyi mlio wa rohoni mrejezeni upya mtu kama huyo kwa roho ya upole, ukijiangalia usije ukajaribiwa wewe mwenyewe.*"

Mtu anapojikuta katika kosa, anajiingiza sana katika kosa hilo na inakuwa vigumu kwake kujitoa peke yake, na anahitaji msaada.

Agizo ni kumsaidia mtu huyo katika jaribio la kumuondoa katika hali aliyonayo, kwa sababu ni dhaifu kuweza kufanya hivyo pekee yake.

Lakini kuna tahadhari kwamba unajiangalia mwenyewe na uwezo wako kwamba usije ukapotea mwenyewe. Wengi wamepotea wanapojaribu kuwaokoa wapendwa wao katika jumba linalounguwa, au katika maji ya barafu baada ya kuanguka katika barafu.

Kuna njia sahihi na njia ambayo sio sahihi ya kufanya chochote.

Mtu anaweza kushawishika kwamba dhambi anazofanya si dhambi kwamba anaweza kujaribu kukushawishi kwamba siyo, na hivyo kukujaribu ili uijaribu na kukusogeza karibu.

"*Rejesha*" katika kifungu halisi ilitumiwa kumaanisha "kurudisha katika muunganiko tena", kama mfupa uliovunjika unavyounganishwa tena na mganga. Hivyo, mrejeze kwa kumfundisha na maonyo ya mara kwa mara.

Lakini Gal. 6:2 ina maana pana.

Tunapaswa kuwasaidia wale walio na mizigo ya huzuni.

- Rum. 12:15, "*Furahini pamoja na wafurahio; lieni pamoja na wafurahio.*"
- 1Kor. 12:26, "*Na kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia nacho, na kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi pamoja nacho.*"

Tunapaswa kuishi maisha sahihi ili kuweza kuwasaidia wengine.

- Math. 5:16, "*Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.*"
- Efe. 5:7-13, "*Basi msishirikiane nao. Kwa maana zamani ninyi mlikuwa giza, bali sasa mmekuwa nuru katika Bwana; enendeni kama watoto wa nuru, kwa kuwa tunda la nuru ni katika wema wote haki na kweli; mkihakiki ni nini impendezayo Bwana. Wala msishirikiane na matendo yasiyozaa ya giza, bali myakemee; kwa kuwa yanayotendeka kwao kwa siri ni aibu hata kuyanena. Lakini yote yaliyokemewa hudhihirishwa na nuru maana kila kilichodhihirika ni nuru.*"
- 1 Yoh. 2:10, "*Yeye ampendaye ndugu yake akaa katika nuru, wala ndani yake hamna kikwazo.*"

Mtwike Bwana mizigo yako

Baadhi ya mizigo iko nje ya uwezo wa kibinadamu na hitaji. Haya yanapaswa kupewa Bwana, kwa sababu katika haya ameahidi kutupatia.

Ataondoa mizigo.

Yesu alikuwa na mzigo wa kutisha wa kubeba na alimuomba Baba yake kuhusu mzigo huu.

- Math. 26:36-39, "*Kisha Yesu akaenda pamoja nao mpaka bustani iitwayo Gethsemane, akawaambia wanafunzi wake , ketini hapa, hata niende kule nikaombe. Akamchukua Petro na wale wana wawili wa Zebedayo, akaanza kuhuzunika na kusononeka. Ndipo akwaambia, Roho yangu inahuzuni nyingi kiasi cha kufa; kaeni hapa mkeshe pamoja nami. Akaendelea mbele kidogo akaanguka kifulifuli, akaomba akisema, Baba yangu, ikiwezekana kikombe hiki kiniepuke, walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe.*"
- Luka 22:42-43, "*akisema, Ee Baba, ikiwa ni mapenzi yako, uniondolee kikombe hiki, walakini si mapenzi yangu, bali yako yatendeke.[Malaika kutoka mbinguni akamtokea akamtia nguvu.*"

Pia Yesu alikuwa na mzigo wa msalaba aliopaswa kuubeba na kushinda mateso yake, lakini alitiwa nguvu ili kwamba aweze kuubeba.

Atakutia nguvu ili uweze kubeba msalaba wako.

Kama jinsi alivyofanya kwa Paulo. 2 Kor.12:7-10, "*Na makusudi nisipate kujivuna kupita kiasi, kwa wingi wa mafunuo hayo nilipewa mwiba katika mwili, mjumbe wa shetani ili anipige, nisije nikajivuna kupita kiasi. Kwa ajili ya kitu hicho nalimsihi Bwana mara tatu kwamba kinitoke. Naye akaniambia, Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu. Kwa hiyo napendezwa na udhaifu, na ufidhuli, na misiba, na adha, na shida, kwa ajili ya Kristo. Maana niwapo dhaifu ndipo nilipo na nguvu.*"

Paulo alikuwa na mwiba kwenye mwili; mara tatu aliomba ili kwamba mwiba huo uweze kuondolewa. Lakini haikuondolewa, ila Mungu alimpa uwezo wa kuubeba.

1 Kor. 10:12-13, "*Kwa hiyo anayejidhania kuwa amesimama na aangalie asianguke. Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu, ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili.*"

Hivyo, kwa mizigo ya maisha inayoshindikana kubebwa, tunapaswa kumtwika Bwana.

- 1 Pet. 5:7, "*Huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu.*"
- Wafil. 4:6-7, "*Msijisumbue kwa neno lolote, bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu ipitayi akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.*"

Mwisho

Hebu na tuwe hiari kuchukulia mizigo ya majukumu kama yetu binafsi; mizigo kama ya wajibu haihamishiki.

Math. 11:29-30, "*Jitieni nira yangu, jifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi.*"

Ebu na tufikirie mizigo ya watu wengine; ile mizigo ambayo tunaweza kuwasaidia wengine kuibeba, kwa ukweli sisi ni walinzi wa ndugu zetu.

Ebu na tumtwike Yesu mizigo ya kukata tamaa, ya uoga, nay a dhambi.

Isa. 53:5-6, "*Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa*

kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; na BWANA ameweka juu yake maovu yetu sisi sote."